

UTARATIBU WA USIMAMIZI WA NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

1.0 Utangulizi

Makala hii inakusudia kuelezea utaratibu wa kusimamia nidhamu katika utumishi wa umma ambapo itabainisha mamlaka za nidhamu na makundi yanayosimamiwa na mamlaka hizo ili kila kundi au mtumishi aweze kupata fursa ya kujua mamlaka yake ya nidhamu ni ipi katika utumishi wa umma. Lengo kuu ni kuimarisha nidhamu katika utumishi wa umma kitu ambacho ni cha msingi katika utendaji wa shughuli za serikali hasa katika utoaji wa huduma za serikali kwa wananchi.

2.0 Utaratibu wa kusimamia nidhamu katika utumishi wa umma.

Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8, 2002 kama ilivyorekebishwa na sheria na. 18, 2007 serikali imeweka utaratibu wa kusimamia masuala ya nidhamu katika utumishi wa umma kama ifuatavyo:

2.1 Rais

Kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 Kanuni Na. 35 (1) , Rais ni Mamlaka ya Nidhamu kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

2.2 Katibu Mkuu Kiongozi

Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kifungu cha 4(3) na Kanuni ya 35(2)(a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 Katibu Mkuu Kiongozi ni mamlaka ya



nidhamu kwa Makatibu Wakuu wote, Manaibu Katibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa , Katibu wa Bunge, Mkurugenzi wa Jiji au Tume, Mkurugenzi wa Uhamiaji, Kamishna wa Zimamoto, Mabalazi na watumishi wengine walioteuliwa na Rais.

2.3 Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa, Makatibu Wakuu, Wakuu wa idara zinazojitegemea, Makatibu Tawala wa Mikoa , Mkurugenzi wa Uhamiaji na Idara ya Utumishi wa walimu

Kwa mujibu wa Kanuni Na. 35(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2003 viongozi hao ni Mamlaka za Nidhamu kwa watumishi wote ambao mamlaka zao za uteuzi siyo Rais. Kwa upande wa Idara ya utumishi wa walimu, kamati za mkoa na wilaya (TSD) zitashughulikia masuala ya nidhamu kwa walimu wote katika maeneo yao kwa mujibu wa Kanuni 121(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2003.

2.4 Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya 2002 ni mamlaka ya nidhamu kwa watumishi wote wa Halmashauri isipokuwa wale walioteuliwa na Rais, Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali ya Mitaa na wale wa Operational Service.

3.0 Majukumu ya Mamlaka za Nidhamu

Kazi kubwa ya mamlaka ya nidhamu ni kusimamia masuala ya nidhamu kwa watumishi wao. Katika utekelezaji wa kazi hii mamlaka za nidhamu zinapaswa kuendesha masuala ya nidhamu kwa kuzingatia Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8, 2002, kanuni na taratibu, miongozo, Nyaraka mbali mbali zinazotolewa na serikali ili kuleta haki na usawa kwa kila mtumishi.



4.0 Hitimisho

Mamlaka za nidhamu zina wajibu wa kusimamia masuala ya nidhamu kwa mujibu wa Sheria, kanuni, miongozo na Nyaraka mbali mbali zinazotolewa na serikali. Aidha watumishi wa umma wanapaswa pia kuzingatia kanuni za maadili ya kazi ili kujenga na kuimarisha nidhamu katika utendaji wa shughuli za serikali.

Ndugu msomaji, iwapo una maswali au maoni tafadhali tuandikie:

Katibu,

Ofisi ya Rais

Tume ya Utumishi wa Umma

Jengo la Acacia, Mtaa wa Samora

S.L.P 9143

Dar es Salaam.

**Simu: +255(22) 2126811/4, 216260 Faksi: +255(22)
2114158**

